

# Kanisa la Kristo Sio Dhehebu

(Sehemu ya Tatu)

1. Bwana wetu hakujiunga na chama au mugawanyiko wakati alikuwa ana tembea pamoja ulimwenguni. Wakati alikuwa ana ishi hapa ulimwenguni, madhehebu manne yalikuwepo ya Wayahudi; Farisayo, Sadukayo, Herodia na Esseni. Lakini madhehebu haya yalifundisha ukweli kidogo, Bwana wetu hakufuata hawa watu.

2. Tena tunafahamu Bwana wetu aliomba kwa umoja, Yh. 17:20-21. Tena Bwana wetu alinunua umoja, ambao ni kinyume na madhehebu, Efe. 2:16. Tena aliomba sana tusiwe na faraka bali tunena mambo, 1 Kor. 1:10. Tena alipanga kwamba tutakuwa na umoja, Efe. 4:1-6. Kwa hiyo Bwana wetu hakuwa na dhehebu na alikuwa kinyume na madhehebu. Kwa hiyo Kanisa lake ni lazima tufuate mapendekezo yake.

## Tupime Kanisa Lililojengwa Na Yesu Na Madhehebu.

Kanisa La Agano Jipya	Madhehebu
(1) Uungu ulianzishwa: Mat. 16:18; Dan. 2:44.	(1) Yanaanzishwa na Wanadamu, bila msaada wa Uungu. Mungu siyo mwandishi wa machafuko, 1 Kor. 14:33. Bwana wetu hakufanya kazi kinyume cha ombi lake la umoja, Yn. 17:20-21.
(2) Litaduma milele: Dan. 2:44; Ebr. 12:28-29.	(2) Yatang'olewa: Mat. 15:13.
(3) Linajulikana kwa majina ya Biblia: Rum. 16:16; Mdo. 20:28; 1 Kor. 1:2.	(3) Yanatumia majina yalio buniwa na wanadamu, au aina ya serikali, siku, sheria fulani. Lakini ni lazima tuseme kama Mausia ya Mungu, 1 Pet. 4:11.
(4) Lilianziswa katika kame la kwanza: Mdo. 2:47.	(4) Katoliki lilianzishwa katika kame ya saba na madhehebu yaliyoanzishwa ili kuwa kinyume cha Katoliki (Protestant) lilianza katika kame ya 16.
(5) Mbinguni ni makao makuu: Efe. 1:22, 23; 1 Pet. 3:22.	(5) Makao makuu yao yapo ulimwenguni, Rumi, Independance, Missouri, Cleveland, Tennessee, Brooklyn, New York, na sehemu nyingi tu.
(6) Linatumia Biblia tu: Mdo. 2:42; 1 Pet. 4:11; Gal. 1:6-9; Ufu. 22:18-19; Yuda 3.	(6) Yanatumia mapokeo, kanuni, vitabu vya imani, katekismo, gazeti na vitabu vingine viliandikwa na wanadamu.
(7) Tunaongezwa katika Kanisa: Mdo. 2:47.	(7) Tunajiunga kwenye madhehebu: lakini tunaongezwa ndani ya Kanisa, 1 Tim. 3:15.
(8) Lazima kwa wokovu: Efe. 5:23; Mdo. 20:28.	(8) Wanadai unaweza kuokolewa bila kuwa mshiriki mwaminifu.
(9) Lilinunuliwa pale Kalvari: Mdo. 20:28; Efe. 5:25.	(9) Hakuna mtu alinunua dhehebu yake kwa kutoa damu lake kwa ajili ya watu wote.
(10) Mitume walikuwa washiriki wa Kanisa hili: Mdo. 2:41.	(10) Hakuna hata mtume moja alikuwa kwenye madhehebu.
(11) Lililochaguliwa na Kristo: Mat. 16:18; Kol. 1:24.	(11) Yamechaguliwa na wanadamu: Zab. 127:1.
(12) Tunaingia kwa kuamini, kutubu, kukiri na kuzikwa ndani ya maji: Mdo. 2:36-47; 8:26-40.	(12) Yana sheria nyingi ya kujiunga: piga kura, lipa fedha, imani tu, neema tu, kunyunyiza, kumwagia. Matendo yale yote yalianzishwa na wanadamu.
(13) Lilianzishwa Yerusalemu: Zek. 1:16; Isa. 2:1-4; Marko 9:1; Luka 24:46; Mdo. 1:1-4.	(13) Yanaanzishwa kila mahali hapa ulimwenguni, siyo Yerusalemu.

**Hitimisho:**

Kanisa la Agano Jipya halifanani na madhehebu. Na ni lazima leo tusijaribu kufanana na madhehebu kwa sababu tukifanya hivyo tutapotea. Yesu alijenga Kanisa Lake, kuwemo ndani yake.